

Maswali

1. Mbona Mungu alikubali mfalme Yabini atawale Israeli?
2. Ni nani alikuwa nabii mwanamke wa Israeli?
3. Mungu alitaka Baraka afanye nini?
4. Heberi na familia yake waliishi wapi?
5. Sisera alifanya nini aliposikia juu ya jeshi la Baraka?
6. Debora alimwambia Baraka nini?
7. Jeshi la Baraka lilifanya nini?
8. Sisera alifanya nini alipokundua ameshindwa?
9. Yaeli alifanya nini?
10. Nani alishinda mfalme wa Kanaani?

Majibu

1. Mungu alimuezesha Yabini kutawala Israeli kwa sababu walikuwa wanafanya maovu.
2. Debora ndiye alikuwa nabii mwanamke.
3. Mungu alitaka Baraka aende mlima wa Tabori na watu 10,000.
4. Familia ya Heberi waliishi Kedeshi.
5. Sisera aliposikia juu ya jeshi la Baraka, alichukua magari 900 ya chuma na kuenda kwa bonde la Kedeshi.
6. Debora alimwambia Baraka kwamba Mungu atampa ushindi.
7. Jeshi la Baraka liliteremka kutoka mlimani na kuua wanajeshi wa Sisera wote.
8. Sisera alipojua ameshindwa alitoroka.
9. Yaeli alitumia nyundo na kigingi cha hema kwa kupiga ndani ya kichwa cha Sisera.
10. Mungu alisaidia Waisraeli kushinda mfalme wa Kanaani.

SHULE YA JUMAPILI YA CBM

Awamu ya 1 Mwaka wa 2



10 Debora na Baraka

Marejeo

Waamuzi 4:1—24

Kiini cha somo


Kwamba Debora na Baraka waliongoza jeshi la Israeli. Mungu aliwasaidia kushinda Sisera. Mungu alisikia maombi ya Waisraeli.

Maneno maalum

1. Israeli + Yabini + katili + Sisera + maombi
2. Nabii + mke + Debora + Baraka + shinda
3. Hema la Heberi + Sisera + magari ya chuma
4. Siku hii ndio siku + chini ya mlima + ua jeshi la Sisera
5. Sisera anatoroka + Yaeli + kunywa
6. Akalala + nyundo na kigingi cha hema + kufa
7. Mungu hujibu maombi + Israeli + angamiza Yabini

10.1 Mara tena Waisraeli walianza kufanya maovu. Mungu hakufurahi kwa hivyo akacha Yabini mfalme wa Kanaani akawatawala. Yabini alikuwa mkatili sana. Jeshi lake liliongozwa na Sisera. Baadaye Waisraeli walimlilia Mungu awasaidie. Mungu alisikia maombi yao.

10.2 Wakati huo Israeli iliongozwa na nabii mke aliyeitwa Debora. Alikuwa muamuzi aliyeamua mabishano ya Israeli yote. Alitumanisha wamwite Baraka mtu wa imani. Akamwambia Baraka, "Bwana Mungu wa Israeli anakuamrisha uchukuwe watu 10,000 na uende mlima wa Tabori. Mungu atakuwezesha ushinde Sisera na jeshi lake katika bonde la Kishoni." Lakini Baraka angeenda tu kama Debora ataenda. Kwa hivyo wakaenda wote Baraka na Debora.




Mungu atakuwezesha ushinde Sisera na jeshi lake katika bonde la Kishoni

10.3 Mtu mmoja aitwaye Heberi na familia yake walijitenga na jamii yao na kujenga hema lao

karibu na Kedeshi. Sisera alikundua kwamba Baraka alikuwa ameenda kwa mlima wa Tabori. Sisera akachukua magari 900 ya chuma. Akaenda na jeshi lake lote kwa bonde la Kishoni.

10.4 Debora akamwambia Baraka, "Siku hii ndiyo Mungu ameweka jeshi la Sisera mikononi mwako." Kwa hivyo Baraka na watu wake 10,000 wakateremka kutoka mlimani. Waliua jeshi la Sisera lote kwa panga zao.

10.5 Sisera alitoroka kutoka vitani. Aliona hema la Heberi. Mfalme Yabini alikuwa rafiki wa kabila la Heberi kwa hivyo alikimbilia huko. Yaeli mke wa Heberi alimkaribisha ndani. Akampa kinywaji. Sisera akamwambia amchungee. "Usimwambie mtu yeyote kwamba niko hapa." Akasema.



10.6 Sisera alikuwa amechoka kwa hivyo akalala upesi. Yaeli alijua kwamba yeye ndiye alikuwa na amri juu ya jeshi la mfalme Yabini. Akachukua nyundo na kigingi cha hema na kukipiga ndani ya kichwa cha Sisera. Yaeli akaenda kumuona Baraka na kumwambia kwamba Sisera amekufa.



10.7 Mungu alijibu maombi kwa kusaidia Waisraeli washinde Yabini mfalme wa Kanaani siku hiyo. Waisraeli waliendelea kuwa na nguvu. Mwishowe waliangamiza Yabini.